

Daily news

WS THURSDAY, AUGUST 14, 2025 Pg 3

PM orders BRT fast-track

Continued from Page 1

requires a large workforce, including drivers.

He called on interested citizens to upgrade their driving skills at the National Institute of Technology (NIT).

Regarding BRT's CNG station, Mr Majaliwa instructed Lake Oil Company, which is implementing the project to complete installation of machines and start providing services.

The new 99 buses are part of the strategic investment by the Mofat Company Limited, a local firm intending to upgrade transport services in the commercial hub by adding a total of 255 new buses valued at about 200bn/-.

Each of the new articulated buses stretches 18-metre long and is powered by natural gases in supporting the country's climate action targets of cutting carbon emissions.

Under the Mofat Company Limited, the new buses will operate the Bus Rapid Transit (BRT) phase two stretching 20.3 kilometres from Mbagala to Gerezani

along Kilwa Road as well as Magomeni and Chang'ombe along Kilwa Road.

In an interview with the Daily News recently, Dar es Salaam Rapid Transport Agency's (DART) Executive Director, Dr Athuman Kihamia said the new buses would commence operation before August 30 this year.

"For the first time in the history of our country, the articulated buses will use natural gases as fuels," he said.

He hinted that currently the new buses at the Dar es Salaam Port are undergoing final logistic procedures.

Dr Kihamia said other 52 brand new articulated buses, property of Mofat Company Limited are en route to Dar es Salaam from China and are expected to arrive within this month.

This transformative investment follows the two contracts inked by DART with the Mofat Company Limited and the Emirates National Group (ENG), an Abu Dhabi-based company and the Mofat Company Limited to boost transport services in the region.

=====

The Standard Thursday 14 August 2025 P41

SGR: 69 technicians leaving for China, 22 listed for Sept

FROM PAGE 1

to handle operations as the railway facility broadens its reach.

The first batch includes 22 train drivers, 34 wagon and locomotive technicians (15 artisan, 15 technical and four mechanical engineers).

Others are 22 operational staff (12 train controllers and 10 transport logistics yard officers), eight business development officers (four in cargo and four in passenger services), he stated.

Also, five safety and security specialists (two technical level officers, one transport officer and two trained engineers) are part of the team, he said.

The training is expected to sharpen technical skills in rolling stock and machinery, strengthen safety in passenger and freight services, improve train control operations, and enhance business efficiency.

"Graduates are expected to return as capacity builders helping to elevate the entire workforce," he suggested, appealing to those leaving to uphold discipline, ethics and patriotism, being ambassadors for TRC and the country as a whole.

Ally Karavina, the TRC board chairman, reiterated a call by President Samia Suluhu Hassan for skilled manpower when launching the Kwana dry port, explaining that those going for training are among the few chosen for this opportunity. "Make it count, and bring home changes the nation can see," he stressed

Eustadius Mlinda of the TRC mechanical department, thanked the government for its support, pledging to share the knowledge with colleagues upon return, while Hayrat Ally, a safety officer, also took deep note of TRC leadership instructions on the mission.

Mwananchi Pg.1 Alhamis 14 Aug 2025

UKAGUZI

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa ndani ya moja ya mabasi mapya kwa ajili ya awamu ya pili ya Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT-2) alipofanya ziara ya kuyakagua pamoja na miundombinu yake, jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk 24 Picha na OWM





Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akikagua mabasi ya awamu ya pili ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT - 2) kwenye Bandari ya Dar es Salaam jana. Wa pili kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

Daily news Thursday August 14 2025 pg 1

PM orders BRT fast-track

By ALLY MAYALA

PRIME Minister Kassim Majaliwa has directed operators of the second phase of the Bus Rapid Transit (BRT) project to work round the clock to ensure the swift completion of infrastructure preparations along the remaining sections of the route, allowing for the immediate commencement of services.

Mr Majaliwa issued the directives yesterday while inspecting the newly acquired 99 buses for the second phase of the BRT and its supportive infrastructures, which include the Mbagala Rangi Tatu BRT Main Station and Gerezani Bus Stop in Dar es Salaam.

He also visited a special designated Compressed Natural Gas (CNG) station

“We want this project to start providing services to Tanzanians especially, Dar es Salaam residents. This project will boost efficiency of the public transport in the Dar es Salaam by bringing modern services, which are safe and fast for the citizens

for the new rapid buses which is under construction at the Mbagala Rangi Tatu Station.

“We want this project to start providing services to Tanzanians especially, Dar es Salaam residents. This project will boost efficiency of the public transport in the Dar es Salaam by bringing modern services, which are safe and fast for the citizens,” Mr Ma-

jaliwa said.

In a related development, Mr Majaliwa directed Executive Director of the Mofat Company Limited, Mr Mohammad Kassim to speed up clearance of the new buses at the Dar es Salaam Port for the operation to kick off.

He said the government is keen to see travel tickets issued electronically rather than

through conventional paper-based methods, as was done in the past.

“By doing that it will be ease for us to monitor the amount of cash collected,” Mr Majaliwa said.

Furthermore, he urged Tanzanians to be proactive in seizing job opportunities arising from the project, which

Continues on Page 3

**Samia
atunukiwa
Tuzo ya
Heshima ya
Maji**

Na Mwandishi Maalum

RAIS Samia Suluhu Hassan ametunukiwa Tuzo ya Juu ya Heshima ya Maji.

Tuzo hiyo imetolewa na Rais wa Jamhuri ya Botswana, Duma Boko na kupokelewa kwa niaba yake na Balizi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, James Bwana.

Tuzo hiyo imetolewa wakati wa Mkutano wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Afrika unaofanyika jijini Cape Town, Afrika Kusini.

Rais Samia ametunukiwa tuzo hiyo kutambua mchango wake mkubwa katika uongozi na mageuzi kwenye sekta ya maji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya maji, usambazaji maji katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ubunifu wa kutafuta fedha za maji kupitia hatifungani ya kijani iliyotolewa na Mamlaka ya Maji Tanga.

Viongozi wengine waliotunukiwa tuzo hiyo kwa kutambua mchango yao katika kuendeleza sekta ya maji kwenye nchi zao ni Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini, Rais Bassirou Diomaye Faye wa Senegal, Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Mtukufu Shehe Mohamed bin Zayed Al Nahyan, Mwanafalme Mohammed bin Salman Al Saudi, Mwanafalme na Waziri Mkuu wa Falme ya Saudi Arabia na Mtukufu Mfalme Letsie III wa Falme ya Lesotho.

Rais mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete ambaye pia ni Mwenyekiti mwenza wa Jopo la Viongozi Mashuhuri katika Uwekezaji kwenye Sekta ya Maji Afrika anashiriki mkutano huo.

Washiriki takribani 600 wa nchi mbalimbali walitaki mkutano huo.

Majaliwa aagiza kasi zaidi miundombinu mwendokasi

Na Mwandishi Maalum

SERIKALI imeagiza waendeshaji wa mradi wa mabasi yaendayo haraka wafanye kazi usiku na mchana kukamilisha maeneo yaliyobaki kuwzesha safari za katikati ya jiji hadi Mbagala kuanza huduma mwezi huu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa agizo hilo alipokagua mabasi mapya kwa ajili

ya awamu ya pili ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT-2) na miundombinu, ikiwemo kituo kikuu cha mabasi hayo cha Mbagala Rangi Tatu na kituo cha Gereza mkoani Dar es Salaam.

Pia, Majaliwa alitembelea ujenzi wa kituo cha kujazia gesi kwa ajili ya mabasi hayo, kinachojengwa katika kituo cha Mbagala Rangi Tatu.

Majaliwa alifuatana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi,

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainab Katimba, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk Jim Yonazi, watendaji wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi (LATRA), Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NTT).

Mradi wa BRT-2 unatarajiwa kuongeza ufanisi wa usafiri wa umma Dar es Salaam na kutoa huduma ya

kisasa, salama na ya haraka kwa wananchi.

Hivi karibuni DART ulisaini mikataba na watoa huduma binafsi kwa ajili ya kuleta mabasi mapya 932 kwa awamu ya kwanza na ya pili hadi ifikapo Oktoba mwaka huu.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk Athumani Kihamia alisema mikataba hiyo ilisainiwa na watoa huduma wanne wakiwemo watatu wa Tanzania.

Dk Kihamia alisema

mabasi 99 yatawasili nchini katikati ya mwezi huu na mengine yatawasili mwezi ujao na ya mwisho yatafika Oktoba mwaka huu.

Alitaja kampuni hizo na mabasi yatakayotewa katika mabano ni Mofat Company Limited (255) ya njia kuu ya urefu wa meta 18, Metro City Link Ltd (334) ya njia za mliso kwa njia tatu na YK City Link Ltd (166) kwa njia sita za mliso na mabasi yote yakiwa ni kwa ajili ya Barabara ya Mbagala.

UKAGUZI

Majaliwa atoa agizo mwendokasi Mbagala



Nasra Abdallah,
Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ametembelea na kukagua miundombinu ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) katika Barabara ya Kilwa na kuagiza kazi iliyosalia ikamilishwe ili huduma hiyo ianze kutolewa mwezi huu.

Majaliwa alifanya ziara hiyo jana, zikiwa zimepita siku sita tangu *Mwananchi* iliporipoti uharifu na kasoro mbalimbali kwenye miundombinu hiyo, ilikamilika miaka miwili iliyopita.

Hali hiyo ilibainika wakati mabasi 99 kati ya 250 yatakayotumika katika awamu ya kwan-

fu wa kilomita 20.3 kati ya Mbagala hadi Gereza, ilijengwa na Kampuni ya Sinohydro China na ilikabidhiwa kwa Dart Agosti 2023.

Katika ziara hiyo Majaliwa aliambatana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi; Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (Tamisemi), Zainab Katimba na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi. Wengine waliokuwapo kwenye msa-

fara huo ni watendaji wa Mamlaka ya Udhubiti Usafiri Ardhi (LATRA), Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART) na Chuo cha Taifa cha Usafiri (NIT) ili kuhakikisha awamu hii inakamilika.

Baada ya kukamilika kwa awamu ya pili ya huo inayohudumia njia ya Mbagala-Gereza, utekelezaji utaelekea kwenye awamu ya tatu. Awamu hii inatarajiwa kushughulikia njia ya kutoka Gereza hadi Gongola la Mboto.

Awamu ya nne itapanua huduma zaidi kwa kuelekea maeneo ya pembezoni na yanayokua kwa kasi jijini, ikiwamo njia ya kuelekea Tegeta kupitia Bagamoyo Road na kuunganisha na Mwenge hadi Ubungo. Miradi hii inalenga kuunganisha wakazi wa pembezoni na mfumo wa ERT, kupunguza muda wa safari na gharama za usafiri. Vilevile, awamu hizi zitaongeza idadi ya mabasi na kupunguza msongamano na muda wa safari.

za kwenye barabara hiyo kati ya Mbagala na katikati ya Jiji la Dar es Salaam, yakiwa yamewasili nchini.

Kwa mujibu wa uchunguzi huo, sehemu mojawapo ambayo ilibainika ina kasoro ni kutokamilika kipande cha Kamata, Kariakoo.

Hata hivyo alipoulizwa Mtendaji Mkuu wa Dart, Dk. Athuman Kihamia alisema mabasi hayo yakianza kazi yatatumiwa barabara za kawaida yanapopita magari mengine kwa sasa hadi hapo njia zake zitakopokamilika.

Mbali na eneo hilo, pia katika vituo hakuna miundombinu ya mageti janja inayoruhusu abiria kukata tiketi wala kuzikagua kidijitali kwa kutumia kadi.

Vilevile baadhi ya miundombinu ilibainika imeanza kuharibika, zikiwamo taa za kuongozea magari huku nyingine zikiwa zimepasuka kwa kile kilichoelezwa ni kutokana na magari yenye urefu mkubwa kupita maeneo hayo, mengi yakiwa ni kutokea bandarini.

Alichosema Majaliwa

Akiwa katika ziara yake leo, Waziri Majaliwa amewataka waendeshaji wa mradi huo kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana kukamilisha maeneo yaliyobaki ili huduma zianze kutolewa.

Katika ziara hiyo pia Waziri Mkuu amekagua mabasi hayo, kituo maalumu cha kujazia gesi kwa ajili ya mabasi hayo, kinachojengwa katika eneo la Mbagala Rangi Tatu.

Mabasi yaliyowasili, mali ya Kampuni ya Mofat, ni sehemu ya mabasi 250 yatakayotoa huduma katika njia hiyo, ikiwa ni utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo, ikiwa imepewa mkataba wa miaka 12. Barabara hiyo yenye ure-

ZAIDI >

Hatua zaanza kuchukuliwa

Maandalizi ya kuanza kwa usafiri wa mabasi yaendayo haraka (BRT) awamu ya pili barabara ya Mbagala-Kilwa yameanza kushika kasi, waki moja baada ya kuwasili kwa mabasi 99 kati ya 250 yatakayotumika katika awamu ya kwanza. Mabasi hayo, yatatumiwa gesi asilia na kutoa huduma kwa mkataba wa miaka 12, katika barabara ya kilomita 20.3 iliyojengwa na Sinohydro ilikabidhiwa kwa Dart tangu Agosti 2023. Mtendaji Mkuu wa Dart, Dk. Athuman Kihamia, amesema huduma inalenga kuanza mwezi huu licha ya mageti janja kutokamilika, ambapo kwa sasa watatumia tiketi kama mpito. Teyari madereva 150 wamepitishwa na waki hii wataanza majaribio ya njia. Wakati mabasi yakiwa bado bandarini, usafi umeanza katika vituo kuanzia Kurasini Ufundi hadi Mbagala.



Majaliwa ataka BRT 2 kazi usiku, mchana

Na MWANDISHI MAALUMU

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewaagiza waendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT-2), kuhakikisha wanafanya kazi usiku na mchana kukamilisha maeneo yaliyobaki yatakayowezesha mradi huo kuanza kutoa huduma haraka iwezekanavyo.

Majaliwa alisema hayo jijini Dar es Salaam, jana, alipokagua mabasi mapya kwa awamu ya pili ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT-2) na miundombinu, kikiwemo Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mbagala Rangi Tatu na Kituo cha Gerezani.

Pia, alitembelea ujenzi wa kituo maalumu cha kujaza gesi kwa mabasi hayo, kinachojengwa katika Kituo cha Mbagala Rangi Tatu.

"Tunataka mradi huu uanze kutoa huduma kwa Watanzania hasa wakazi wa Dar es Salaam, mradi huu utaongeza ufanisi wa usafiri wa umma katika jijini la Dar es Salaam na kutoa huduma ya kisasa, salama na ya haraka kwa wananchi," alisema.

Majaliwa alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni

ya utoaji huduma ya usafiri ya Mofat Mohammad, kuhakikisha anakamilisha haraka uwaratibu za utoaji wa mabasi 99 yaliyopo bandarini kuwezesha huduma hiyo kuanza kwa wakati.

Alisema serikali inataka kuona awamu ya pili ya mradi wa BRT, tiketi za usafiri kupitia mabasi hayo zinakuwa za kielektroniki badala ya tiketi za karatasi kama ilivyokuwa awali.

"Tukifanya hivi itatusaidia kumonitor (kusimamia) kiasi cha fedha kinachokusanywa," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa za ajira zitakazotokana na mradi huo zikiwemo udereva.

"Nendeni mkasome masuala ya udereva kupitia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), mradi huu utahitaji idadi kubwa ya madereva wenye ujuzi," alisema.

Akizungumza baada ya kukagua kituo cha kujaza gesi katika mabasi hayo kilichopo Kituo Kikuu cha Mbagala Rangi Tatu, Majaliwa alitaka Kampuni ya Lake Oil inayotekeleza mradi huo kuhakikisha wanakamilisha usimikaji wa mitambo waanze kutoa huduma.

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa akikagua Kituo Kikuu cha Mabasi Yaendayo Haraka(BRT), Barabara ya Kilwa Mbagala Rangi Tatu jijini Dar es Salaam, jana. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu).

+

Zanzibar Leo

AMBUZI

Alkhamis 14 Agosti, 2025

5

KERO



BAADHI ya waendesha boda boda hawaheshimu sheria za usalama barabarani kwa kupakia abiria zaidi ya mmoja.

Ajali za barabarani bado tatizo Mjini Magharibi

MIZA RAMADHAN NA RAHMA ABDALLA, SUZA

JESHI la Polisi mkoa wa Mjini Magharibi limesema watu 11 wamefariki kutokana na ajali za barabarani katika mwezi wa Julai, 2025 ikiwa zimeongezeka ikilinganishwa na miezi iliyopita.

Akizungumza na Zanzibar Leo, Kaimu Kamanda wa polisi mkoani humo, Kamishina Msaidizi wa Polisi (ACP), Abubakar Khamis Ali, alisema kuwa ajali hizo zimesababishwa na mwendokasi wa madereva wa gari za abiria na bodaboda.

Alifafanua kuwa kwa upande wa wilaya ya Mjini kuliripotiwa ajali mbili, wilaya ya Magharibi 'A' ajali tano na Magharibi 'B' zilitokea ajali nne ambazo mbali ya vifo, zilisababisha majeruhi mbali mbali kwa watu wazima, waenda kwa miguu, wapanda bodaboda na watoto.

Hata hivyo alieleza kuwa

ikilinganishwa na miezi mengine, ajali zilizoripotiwa kwa mwezi huo zilikuwa ongezeko lake lilikuwa sio kubwa kutokana na jitihada zinazozofanywa na jeshi la polisi za kupunguza ongezeko la ajali hizo.

ACP Abubakar aliongeza kuwa uchunguzi wa awali wa sababu za ajali hizo hizo ni matumizi mabaya ya vyombo vya moto zikiwemo bodaboda ambazo ndio zinaoongoza kwa ajali na uzembe wanaotumia kilevi wakiwa wanaendesha chombo cha usafiri.

Alielezea kuwa madereva wa gari za abiria wanaoendesha gari kwa fujo na kutozingatia sheria za barabarani ambao husababisha ajali za barabarani.

Sambamba na hayo, alitoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto na kuwataka wasiwe wazembe na wazingatie sheria za barabarani wakati wanapoendesha gari pamoja na kuzingatia wanaotembea kwa miguu ili waepushe ajali za ovyo.

Hata hivyo aliwataka wanaoemi

waweze kuwa makini wakati wanapo tembea barabarani na kulinda usalama wao kabla ya kulindwa wao.

Akizungumzia hali hiyo, mkaazi wa Kwahani, Ibrahim Nyange Silima, alishauri kwa madereva wanaotumia vyombo vya moto wawe na uwangalifu kwa wanao kwenda kwa miguu.

Pia aliwataka madereva hao kufuata alama za barabarani kwa mujibu zilivyoekwa na Jeshi la Polisi na hali hii itapelekea kuepusha ajali za barabarani kwa kiasi kikubwa.

Kwa upande wake, Salma Khamis Juma, mkaazi wa Michenzani aliliomba jeshi la polisi liwe na mkakati mzuri kwa wanaoendesha vyombo vya moto barabarani ili kupunguza ajali na vifo.

Hivyo alifahamisha kuwa kufanya hivyo kutakuwa ni chanzo cha kupunguza ajali na hata kwa bodaboda itakuwa vizuri kwa kuwafanya wasiendeshe kwa mwendo kasii wakiwa barabarani.